# PRECIOUS SERIES 2021

## KISWAHILI : LUGHA

STEPPING - IN **6**

**001**

*SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI*

*1. Hakikisha umeandika*
*(i)Jina lako* *(ii)Jina la shule yako*

***MUDA: SAA 1 DAK. 40***

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 - 15. Kwa kila nafasi, chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale manne uliyopewa.**

Mchezo ___1___ kandanda hupendeza sana. Mchezo ___2___ hushirikisha timu ___3___ kwa wakati mmoja. Kila timu huwa na ___4___ kumi na ___5___. Timu zenyewe huvaa ___6___. ___7___ ni mavazi ya kujitambulisha uwanjani. Pia wachezaji wale huvaa viatu maalum vya ___8___.

1. A. wa B. ya C. za D. la
2. A. hii B. huyo C. hiyo D. huu
3. A. tatu B. nne C. moja D. mbili
4. A. waimbaji B. wachezaji C. wakimbiaji D. waogeleaji
5. A. moja B. watatu C. mmoja D. wawili
6. A. sare B. matambara C. kanga D. wawili
7. A. Hizi B. Hii C. Hili D. Haya
8. A. zoka B. soga C. soka D. zoga

Mwanafunzi anapaswa kusoma ___9___ bidii shuleni. Ni vyema azingatie ___10___ ya ___11___. Asipotii sheria za shule, bila shaka ___12___ mtihani. Pia, ___13___ na wanafunzi wenzake. Mwisho, afanye ___14___ yake kwa ___15___.

19. A. kwa B. na C. kuwa D. kua
10. A. maagizo B. miigizo C. maigizo D. maongozi
11. A. mpishi B. mkulima C. mwalimu D. mnunuzi
12. A. atapasi B. hatafeli C. atashinda D. atafeli
13. A. adharauliane B. agombane C. apendane D. achukiane
14. A. kasi B. kazi C. kisi D. kisa
15. A. uangalifu B. uzembe C. uharibu D. uchukivu

**Kutoka swali la16 - 30, chagua jibu sahihi.**

16. Mtu akikuambia ***"usiku mwanana"*** utamjibu

A. vyema B. majaliwa

A. sijambo D. asante

17. **Tegua kitendawili hiki:-**

Ngozi ndani nyama nje

A. firigisi B. jeneza

C. jiwe D. moto

18. **Tumia kivumushi sahihi kujaza pengo;**

Chai ________ imepikwa ikapikika.

A. yenyewe B. chenyewe

C. lenyewe D. zenyewe

19. **Andika sentensi hii katika hali ya udogo:-**

Mkono unauma

A. jikono linauma B. kimkono kinauma

C. kikono kinauma D. kono kinauma

20. **Kamilisha tashbihi hii:-**

Nyeupe kama

A. theluji B. meno

C. maziwa D. mbao

21. Andika akisami $^1/_7$ kwa maneno

A. sudusi B. robo

C. subui D. humusi

22. **Kamilisha methali hii:-**

Jina jema hung'aa

A. shuleni B. mbinguni

C. mezani D. gizani

23. **Chagua wingi wa:-**

Nitakununulia kitabu

A. Nitawanunulia kitabu

B. Tutawanunulia kitabu

C. Tutawanunulia vitabu

D. Watawanunulia vitabu

24. Chagua matumizi ya majina ya makundi yaliyosahihi:-

A. Biwi la takataka

B. Safu ya nguo

C. Halaiki ya milima

D. Mlolongo wa barabara

25. Malipo yatolewayo shuleni ili mwanafunzi apate kufunzwa ni

A.nauli B. karo

C. kiingilio D. rushwa

26. Chagua neno ambalo si la kundi moja na mengine;

A. ngao B. mkuki

C. manati D. ngoma

27. Msimu wa baridi nyingi huitwa

A. kipupwe B. ukame

C. kusi D. vuli

28. Utamwitaje dada ya mama yako?

A. Shemeji B. Halati

C. Mjomba D. Shangazi

29. Andika neno <u>**somo**</u> katika kauli ya kutendea

A. somwa B. somewa

C. somea D. somesha

30. Nomino **'chura'** iko katika ngeli gani?

A. I - ZI B. LI - YA

C. U - ZI D. A - WA

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Serikali inapaswa kuwaelimisha wakulima nchini. Hii ni kwa sababu ya upungufu wa mazao ya kilimo. Wakulima wengi wamepungukiwa na ujuzi wa shughuli za ukulima.

Hivyo basi, kuna haja ya kuwafunza njia za kunyunyizia mimea yao dawa. Pia, inafaa wafunzwe kuhusu njia za upanzi zifaazo. Kwa wengine, kutumia mbolea huwa ni jambo wasilolijua wala kulithamini. Hii hupunguza mazao ikiwa mashamba hayana rutuba.

Kwa wale wanaofuga wanyama na ndege kama vile kuku, wanapaswa kufundishwa kuhusu magonjwa. Kwa mfano, ng'ombe huvamiwa na ugonjwa wa miguu na midomo na pia sotoka. Kuku nao huvamiwa na ugonjwa wa kuhara, jambo ambalo linaweza kumaliza kizimba kizima.

Hivyo basi, maafisa wa kilimo hawana budi kuwa mstari wa mbele katika kuwapa wakulima misaada ya kila aina. Hii ni kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu.

**31.** Ni akina nani wanapaswa kuelimisha na serikali?

A. Wanafunzi B. Wananchi
C. Wakulima D. Maafisa wa kilimo

**32.** Kwa nini mazao ya kilimo yamepungua?

A. Wakulima hawafanyi bidii
B. Wakulima hawana ujuzi wa kulima
C. Kuna upungufu wa mvua
D. Kuna ukame

**33.** Wakulima ambao mashamba yao hayana rutuba hawatumii

A. maji
B. dawa za kuua wadudu
C. njia mwafaka za upanzi
D. mbolea

**34.** Ni mnyama yupi huugua sotoka?

A. Ng'ombe B. Kuku
C. Mkulima D. Serikali

**35.** Ndege kama vile kuku hufugwa wapi kulingana na taarifa?

A. Zizini B. Kizimbani
C. Shambani D. Kiotani

**36.** Maneno ***'kumaliza kizimba kizima'*** yana maana gani?

A. Kuharibu kizimba chote
B. Kubomoa kizimba chote
C. Kuwaua ng'ombe wote
D. Kuwaua kuku wote

**37.** Wakulima wanahitaji kupewa

A. mbolea
B. dawa
C. msaada wa kila aina
D. ng'ombe na kuku

**38.** Kuku huangua kifaranga, ng'ombe huzaa

A. kang'ombe B. king'ombe
C. ndama D. mwanang'ombe

**39.** Kilimo ni nini kulingana na taarifa?

A. Ngao maishani
B. Uchumi wa nchi
C. Ng'ombe na kuku
D. Uti wa mgongo wa taifa letu

**40.** Chagua kichwa kifaacho taarifa hii bora zaidi;

A. kilimo cha ufugaji
B. aina za kilimo
C. kilimo cha upanzi wa mimea
D. elimu kwa wakulima

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Katika mtaa wa Maajabu, kulikuwa na mvulana kwa jina Kosaadabu. Mvulana huyu alikuwa mtoto wa ajabu kupindukia. Kwa vile alivyokuwa mwana wa pekee katika familia yao, alidekezwa kama yai. Wavyele wake hawakukubali kusikia kuwa Kosaadabu amecharazwa shuleni.

Wazazi hawa walimtumia mfanyikazi wao kucharazwa kwa niaba ya mwanawao. Mfanyikazi huyo aliitwa Mateso. Kila mara, Kosaadabu alipofanya kosa lolote aliyecharazwa viboko alikuwa Mateso.

Siku moja, mzee Mateso aliyekuwa amekula chumvi nyingi, alikuwa karibu kupigwa kalamu kwa kukataa kupigwa. Siku hiyo, mwalimu mkuu alikataa katakata kumpiga mzee yule na kwa mara ya kwanza, Kosaadabu akaonja kijiti.

Baada ya kusalimiwa na fimbo ya mwalimu mkuu, Kosaadabu akakataa shule. Sasa hivi amekuwa kijana wa mtaani anayerandaranda tu kwa kukosa elimu.

**41.** Kosaadabu aliishi wapi?
A. Katika kijiji cha Maajabu
B. Shuleni
C. Kwa akina Mateso
D. Katika mtaa wa maajabu

**42.** Kwa nini Kosaadabu alitunzwa kama yai?
A. Alikuwa mwana wa pekee
B. Alipendwa sana
C. Alikuwa mdogo
D. Alichukiwa na walimu

**43.** Ni nini wazazi wake Kosaadabu hawakutaka kusikia?
A. Kuwa Mateso amekataa kuchapwa
B. Kuwa Mateso amechapwa
C. Kuwa mwana wao amechapwa
D. Kuwa mwana wao amefukuzwa shuleni

**44.** Maneno ***'Mateso alicharazwa kwa niaba ya Kosaadabu,"*** yana maana gani?
A. Mateso alichapwa badala ya Kosaadabu
B. Kosaadabu alichapwa baada ya Mateso
C. Mateso ndiye aliyechapwa kwa kufanya makosa
D. Kosaadabu aliadhibiwa kwa kuchapwa

**45.** 'Kula chumvi nyingi' ni nahau iliyo na maana ya
A. kula chakula chenye chumvi nyingi
B. kupenda kula chumvi nyingi
C. kuwa na umri mdogo
D. kuwa ameishi miaka mingi

**46.** Mateso alipokataa kuchapwa
A. mwalimu mkuu alikasirika
B. alikuwa karibu kufutwa kazi
C. alifutwa kazi
D. aliajiriwa kazi shuleni

**47.** Kwa nini Kosaadabu alikataa shule? Kw sababu
A. alisalimiwa na mwalimu mkuu
B. alichapwa kwa mara ya kwanza
C. alisalimia fimbo
D. mzee Mateso alikataa kuchapwa

**48.** Sasa Kosaadabu
A. ni tajiri mkubwa
B. ni mwenda wazimu
C. anaishi kwa raha
D. ni ombaomba

**49.** Ni kweli kusema kuwa Kosaadabu aliharibiwa na
A. wazazi wake
B. mwalimu mkuu
C. Mateso
D. rafiki zake

**50.** Ni methali gani inayoweza kuelezea taarifa hii bora zaidi?
A. Baada ya dhiki ni faraja
B. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
C. Dawa ya moto ni moto
D. Akiba haiozi